

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

MKOA WA DODOMA

Tel.: 2354817
Fax: 2354817/ 2321550



Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji,
1 Mtaa wa CDA,
S.L.P. 1249,
41182 DODOMA.
Baruapepe: cd@dodomacc.go.tz

Kumb. Na. HJD/I.10/8/18

Tarehe: 09 Novemba, 2020

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anapenda kuwatangazia waombaji wenyewe sifa kujaza nafasi za kazi katika kada ifuatayo;

1.0 MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA NAFASI MOJA (1)

SIFA ZA MWOMBALI

- Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa ya Kidato cha Nne au cha Sita na awe na Shahada ya Utawala au Sheria katika mojawapo ya fani za Utawala wa Umma au Sheria.
- Awe na uzoefu usiopungua miaka kumi (10) katika masuala ya Utawala na Sheria.

MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira
- (ii) Kuendesha vikao vyote vya Bodi ya Ajira kwa kufuata Kanuni, Sheria na Taratibu zilizopo
- (iii) Kufungua vikao vya Bodi ya Ajira pamoja na kufunga

MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.
2. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote, waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**)
4. Maombi yote waombaji yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (**Kidato cha IV au VI**), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
5. Testimonial ***"provisional results"* "statement of results"** hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (**FORM FOUR AND FORM SIX RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**

6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (**TCU na NECTA**) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma wanaruhusiwa kuomba.
8. Hakutakuwa na mshahara kwa mwezi, Mwenyekiti wa Bodi atalipwa posho ya kikao kwa kila kikao kitakapofanyika.
9. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
10. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 20 Novemba, 2020 saa 9:30 Alasiri
11. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta au kupitia Masjala Kuu ya Jiji (**Chumba Namba 74**) kwa anwani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji la Dodoma,
S.L.P 1249,
DODOMA
Barua Pepe: cd@dodomacc.go.tz**



Joseph C. Mafuru
**MKURUGENZI WA JIJI
DODOMA**